

Mvua inapokuja:



Iwapo kuna mavuno mazuri au hamna hata kidogo:

Yote ni uamuzi wa mkulima.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Musembi D.K.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kiboko

S.L.P. 12-901380, Makindu

Simu: 045 22366/7/8

Nukulishi: 045 622314

Baruapepe: karikiboko@yahoo.co.ke

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 29 /2008

Shilingi 20 za Kenya

Panda mapema ili kuongeza mavuno katika sehemu kame



Utangulizi

Ukosefu wa mvua ya kutosha ni tatizo sugu miongoni mwa wakulima wa nyanda za kusini Kenya.

Hata hivyo tatizo hili linazidishwa na baadhi ya wakulima ambao mtindo wao huifanya kuwa vigumu kuzalisha mazao mazuri kutokana na mvua ndogo inayopatikana.

Kuchelewa kutayarisha shamba

Mvua hunyesha kabla ya wakulima wengi kutayarisha mashamba yao ili kupanda mimea au nyasi. Wakulima wasiopenda kupalilia husubiri magugu kumea ili wapande huku wakiyalima magugu hayo.

Mtindo huu unasababishwa na kutoelewa namna ya mvua katika nyanda za kusini na husababisha hali mbaya kuwa mbaya zaidi.

Kuelewa mvua

Kwa kila kipindi, mvua hunyesha kwa kiwango mahsusi kama ilivyo kuwa kuna kiwango maalum katika glasi iliyojaa maji.

Katika wilaya ya Makeni kiwango hiki maalum ni takribani milimita 290 wakati wa msimu mfupi wa mvua (nthwa) au milimita 180 wakati wa mvua ya masika (una).

Kuna wakati ambapo mvua huzidi kiwango hiki maalum kama ilivyokuwa wakati wa El Nino (1977) au mvua ya Nthwa (2006).

Wakati mwingine kiwango hiki hupungua kama ilivyokuwa wakati wa La Nina, mwaka 2000 au mvua ya una ya 2007.

Kukuza mimea

Ikiwa kiwango cha mvua ni maalum kama ilivyo gilasi ya maji, ina maana kuwa mimea iliyopandwa kabla ya au mwanzo wa mvua itatumia maji yote ya mvua au gilasi iliyojaa ya maji. Matokeo yake yatakuwa ni mavuno mazuri.



Mavuno mazuri

Hata hivyo, mvua ikianza kunyesha kabla ya kupanda au wakulima wanaposubiri magugu yakue ili wachimbe huku wakipanda, mimea itakayopandwa hupata chini ya kiwango maalum cha mvua (pengine nusu ya mvua) kinachopatikana kwa ukuaji katika kipindi hicho na kwa hivyo huenda mimea ikafeli.



Mavuno mabaya

Hii ina maana kuwa mimea inayopanda baada ya mvua kuanza huenda ikafeli na kukasirisha ilihali mimea iliyopanda kabla ya au mwanzo wa mvua huenda ikafanikiwa na kukupatia mavuno mazuri.

Kwa hivyo, ni uamuzi wako kupanda mapema na kuwa na mavuno mazuri au kuchelewa kupanda na kuwa bila mavuno yoyote.